# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA ARDHI NA MAWASILIANO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**FEBRUARI, 2018**

**RIPOTI YA KAMATI YA ARDHI NA MAWASILIANO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

# SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi ni moja wapo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya 106(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, (Toleo la 2016).

Kazi na majukumu ya Kamati hii yamebainishwa na kufafanuliwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

(a) Kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
(b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotowa katika Baraza.
(c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi katika Wizara husika.
(d) Kuchunguza na kufuatilia Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
(e) Kuchambua Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka.
(f) Kushughulikia Miswada ya Sheria inayokabidhiwa kwake na Spika.
(g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekeleaji wa ahadi hizo.
(h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ambapo katika ripoti hii inajulikana kama “Kamati” ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Wizara mbili za Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Idara, Mashirika, Mamlaka na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo. Wizara zifuatazo zinasimamiwa na Kamati hii:

(i) Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

(ii) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

## 1.1 WAJUMBE WA KAMATI

Kamati hii inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Suleiman Sarhan Said | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Khadija Omar Kibano | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Said Omar Said | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 10. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |

## 1.2 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa malengo yafuatayo:

(a) Kufuatilia Maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2016/2017.
(b) Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2016/2017.
(c) Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka 2017/2018.

(d) Kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara katika taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita kama ifuatavyo:

(i) Tanzania Bara, kuanzia tarehe 14/08/2017 hadi tarehe 25/08/2017.

(ii) Pemba, kuanzia tarehe 13/11/2017 hadi tarehe 24/11/2017.

(iii) Unguja kuanzia tarehe 15/1/2018 hadi tarehe 26/1/2018.

Aidha, Kamati kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ilibahatika kutembelea Taasisi mbalimbali Tanzania Bara kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili kutoa fursa kwa wajumbe kujifunza kwa vitendo na hatimae kuweza kuishauri Serikali ipasavyo.

Kamati ilitembelea Mradi wa Ujenzi wa ‘Terminal III’ Tanzania Bara, Mamlaka ya Hali ya Hewa, Makao Makuu Tanzania Bara, Shirika la Nyumba Tanzania Bara (NHC), Shirika la Ndege la Tanzania “Air Tanzania”, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (SUMATRA), Chuo cha Ubaharia pamoja na kufanya ziara ya kimafunzo katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA) na Mamlaka ya Maji (DAWASA).

Sambamba na hayo, katika kuhakikisha ufanisi wa masuala mbali mbali yanayogusa Wizara zinazosimamiwa na Wizara hizi mbili, Kamati iliwakutanisha Viongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Tanzania Bara na Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar ili kuzungumzia suala zima la ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kwa baadhi ya miradi inayokusudiwa kutekelezwa Zanzibar pamoja na Changamoto ya kutotambuliwa kwa Chuo cha Ubaharia kilichopo Zanzibar (DANOUS).

Vile vile, Kamati ilipanga kukutana na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ila kwa bahati mbaya Katibu

Mkuu huyo hakuwa tayari kukutana na Kamati ili kupata ufafanuzi kwa masuala mbali mbali yanayohusu changamoto za kifedha na kiutendaji ikiwemo miradi mbali mbali iliyokwama kwa siku nyingi ambayo inahitaji ridhaa ya Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo Barabara ya Wete - Chake pamoja na madeni ya Umeme kwa "ZECO" kwa taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar ambayo yanarejesha nyuma jitihada za "ZECO" kujikwamua na changamoto zinazoikabili katika majukumu yake ya kila siku.

Pamoja na hayo, Kamati pia ilikutana na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje kwa lengo la kuzungumzia maswali mbali mbali yanayohusu upande wa Zanzibar ambayo ni ya Muungano hususan katika sehemu ya mambo ya nje.

## 1.3 **HADIDU REJEA**

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2017/2018, Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo:

(a) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.
(b) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.
(c) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, (Toleo la Mwaka 2016).
(d) 'Hansard' za Baraza za Mwaka 2016/2017.
(e) Ripoti za Kamati kwa Mwaka 2016/2017.
(f) Hotuba za Bajeti za Taasisi za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii.

# SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA

### 2. UTANGULIZI

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ni Wizara muhimu katika mfumo wa utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, Wizara hii ina dhamana ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafaidika na huduma bora za maji, matumizi bora ya ardhi, usimamizi na utunzaji wa mazingira pamoja na upatikanaji bora wa huduma za nishati iliyo salama na endelevu kwa ustawi wa maisha ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Wizara hii imeundwa na sekta kuu tano ambazo ni Mipango, Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ambazo hutekelezwa kupitia programu kuu nne.

(a) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi.
(b) Programu ya Usimamizi na Upangaji wa Matumizi ya Ardhi.
(c) Programu ya Usimamizi wa Huduma za Majina Nishati.
(d) Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

### 2.1 SEKTA YA MIPANGO NA UENDESHAJI

Sekta hii imegawika kama ifuatavyo:

(a) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
(b) Idara ya Utumishi na Uendeshaji.
(c) Afisi Kuu Pemba.

Kamati imegundua kwamba jukumu kubwa la sekta hii ni kuratibu na kusimamia Sera, Mipango na Shughuli zote za kawaida na za maendeleo za Wizara husika.

### 2.1.1CHANGAMOTO

**Ufinyu wa Bajeti:** Idara hizi licha ya kubeba majukumu makubwa ya shughuli za uendeshaji wa Wizara nzima lakini bado bajeti inayotengewa ni finyu hali ambayo inapelekea baadhi ya shughuli kutokutekelezwa ipasavyo kama zilivyopangwa kwa mwaka wa bajeti husika.

## 2.2 SEKTA YA ARDHI

Sekta ya Ardhi ndani ya Wizara hii imeundwa kwa Idara na Taasisi zifuatazo:

(a) Idara ya Ardhi na Usajili (Mahakama ya Ardhi, Afisi ya Mrajis wa Ardhi na Bodi ya Uhaulishaji).
(b) Idara ya Upimaji na Ramani.
(c) Idara ya Mipango Miji na Vijiji.

Idara na Taasisi hizo kwa pamoja zinaunda Kamisheni ya Ardhi inayoongozwa na Katibu Mtendaji ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Idara hizo.

### 2.2.1 KAMISHENI YA ARDHI

Kamisheni ya Ardhi ni wakala wa Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria Namba 6 ya mwaka 2015. Madhumuni ya kuanzishwa kwake ni kusimamia utawala wa ardhi na kupanga matumizi bora ya ardhi. Aidha, haki ya kulinda rasilimali muhimu ya ardhi iliyo chache na isiyoongezeka kwa maslahi ya Taifa na maendeleo ya jamii ni jambo la msingi lililozingatiwa katika uanzishwaji wa Kamisheni ya Ardhi Zanzibar. Pia, Kamisheni ya Ardhi ni mshauri na msimamizi mkuu wa maswali ya ardhi.

Sambamba na hilo, Kamisheni ya Ardhi inaundwa na Idara nne kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 6(2) cha Sheria ya Kamisheni. Idara hizo ni: Idara ya Ardhi, Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Upimaji na Ramani na Afisi ya Msajili/Mrajis wa Ardhi.

### 2.2.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KAMISHENI YA ARDHI

Kamisheni ya Ardhi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Uelewa mdogo wa baadhi ya taasisi za Serikali kuhusiana na Mamlaka ya Usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni ya Ardhi hususan katika ugawaji na upangaji wa matumizi ya ardhi.

2. Upungufu wa wafanyakazi wenye utaalamu wa usimamizi Ardhi, Uthamini Ardhi, Mipango Miji, Upimaji na Uchoraji pamoja na ukosefu wa vifaa vya kisasa.

3. Kuwepo kwa bajeti ndogo ya kukidhi mahitaji halisi ya kuendeshea shughuli za Kamisheni.

4. Kuwepo ardhi kubwa ambayo bado haijafanyiwa utambuzi na kusajiliwa kulingana na malengo yaliowekwa.

5. Kuwepo kwa Mamlaka mbili tofauti katika usimamizi wa ardhi za Eka Tatu kwa Unguja na Pemba.

6. Kiwango kidogo cha uelewa wa jamii juu ya dhana ya matumizi, utawala na usimamizi wa ardhi kwa mujibu wa Sheria na miongozo.

7. Kutokuwepo kwa mashirikiano baina ya taasisi za Serikali katika utekelezaji mipango na matumizi bora ya ardhi.

8. Uchelewaji wa uingizaji wa OC kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa Wizara zote, jambo linalopelekea taasisi za Serikali kushindwa kutekeleza kazi walizopangiwa kwa wakati.

9. Kamisheni kupatiwa fungu moja la OC kwa Idara zake nne yaani Afisi ya Mrajis wa Ardhi, Kamisheni ya Ardhi, Idara ya Upimaji na Ramani, na Idara ya Upimaji na Ramani. Hii hukwamisha shughuli za kazi zao kwani kila Idara inamajukumu yake.

10. Afisa mtambuzi wa Ardhi alieteuliwa na Waziri kwa mujibu wa Sheria iliyounda Kamisheni ya Ardhi hadi hivi leo hajalipwa stahiki zake tangu ateuliwe. hili ni suala la ukiukaji wa Sheria.

11. Kamisheni inakabiliwa na ukosefu mkubwa wa usafiri yaani magari kwa taasisi zake zote wakati kazi zao nyingi ni za nje ya Ofisi yaani ni za ufuatiliaji zaidi.

12. Kamisheni kushindwa kumpatia "Lease" Muekezaji mzalendo aliyewekeza Ujenzi wa Chelezo na "Slipway" kwa ajili ya ukarabati wa Boti na Meli huko Mangapwani. Hii inatokana na ubinafsi wa watu wachache kwa maslahi yao pamoja ya kuwa ripoti ya Mazingira imeruhusu mradi huo kutekelezwa katika eneo hilo.

### 2.2.3 **MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaipongeza Wizara kupitia Kamisheni ya Ardhi kwa kuvuka malengo ya makusanyo yanayotokana na kodi mbalimbali za ardhi kwa kufikia Shilingi za Kitanzania 1,350,556,156.28 mwezi wa Disemba, 2017 ambazo ni sawa na 164% ukilinganisha na miaka ya nyuma 2016/2017.

2. Aidha, Kamati inaipongeza tena Serikali pamoja na Wizara husika kwa kuanzisha uwekaji wa kumbukumbu wa taarifa za ardhi katika mfumo wa "Data Base" jambo ambalo litasaidia kupunguza idadi ya nyaraka zisizo halali pamoja na migogoro ya ardhi. Pia, utoaji wa kiwanja kimoja kumilikishwa watu wawili tofauti pamoja na kuondoa migogoro ya ardhi ambayo imekua ni tatizo sugu hapa Zanzibar.

3. Kamati inaiomba Serikali kuipatia 5% Kamisheni ya Ardhi ya mapato wanayokusanya kutokana na kodi za ardhi badala ya kuziingiza fedha zote hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Hazina). Hali hii inapelekea kusubiria mgao kupitia OC ambapo hupatiwa fedha kidogo ambazo huchelewesha utekelezaji wa kazi za Idara hiyo.

4. Vile vile, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi kuandaa mpango maalumu wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya dhana nzima ya utambuzi na usajili wa ardhi kwa Unguja na Pemba.

5. Kutolipwa kodi ya matumizi ya ardhi kwa baadhi ya Makampuni ya Simu za Mkononi ambapo kwa mujibu wa kumbukumbu kutoka kwa wakala wa ukusanyaji kodi (ZRB), jumla ya mikataba 175 ambayo haikufanyiwa malipo, mikataba 80 ni ya Kampuni ya Simu za Mkononi ya Zantel jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za Serikali.

6. Kamati inaitaka Serikali kuipatia OC kila Idara iliyoko chini ya Kamisheni ya Ardhi kwani majukumu yao ni makubwa na kila siku wanahitaji bajeti iliyo madhubuti na ya uhakika.

7. Kamati inaitaka Serikali kumlipa stahiki zake pamoja na malimbikizo yake Afisa Mtambuzi wa Ardhi.

8. Kamati inaitaka Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kupitia Kamisheni ya Ardhi kuandaa utaratibu maalum wa usimamizi wa maeneo yote ya Eka Tatu kwa upande wa Unguja na Pemba. Kwani hadi Kamati inapokea taarifa hii masuala hayo yanasimamiwa na Wizara mbili tofauti, ambapo kwa upande wa Unguja Msimamizi Mkuu wa masuala ya Ardhi ni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na kwa upande wa Pemba masuala haya yanasimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hali inayopelekea mgongano wa madaraka na mgawanyo wa kazi.

9. Kamati inaitaka Serikali kuipatia Kamisheni ya Ardhi magari ya kutosha kwa Idara zake zote ili kuweza kutimiza malengo yao kwa wakati kama walivyoomba katika bajeti zao.

10. Kamati inaitaka Kamisheni ya Ardhi kumpatia “Lease” mkaazi Mzalendo aliejenga Chelezo huko Mangapwani kwani ni miradi ambao utaleta tija kubwa kwa taifa hasa kwa vyombo vitakavyohitaji matengenezo ikiwemo meli zetu za Serikali na Binafsi badala ya kuzipeleka Mombasa kwa ajili ya matengenezo hayo.

### 2.2.4 **MAHAKAMA YA ARDHI**

Mahakama ya Ardhi ni moja kati ya taasisi muhimu iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya mwaka 1994 ambayo inasimamiwa na Sekta ya Ardhi hapa Zanzibar. Aidha, lengo kuu la kuanzishwa kwa Mahakama hii ni kupokea, kusikiliza na kuamua kesi mbalimbali zinazohusiana na migogoro ya ardhi inayofikishwa katika Mahakama hizo kwa Unguja na Pemba. Katika kipindi ambacho Kamati ilipotembelea, jumla ya kesi 108 zimeshasikilizwa na kutolewa maamuzi. Hii ni sawa na asilimia 154.

#### 2.2.4.1 **CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAHAKAMA YA ARDHI**

Mahakama ya Ardhi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Ufinyu wa Bajeti iliyopelekea kupunguza ufanisi wa kazi za Mahakama hiyo kwa upande wa Unguja na Pemba kwa kushindwa kupata vitendea kazi kama vile vifaa vya kuandikia, karatasi, kalamu, kompyuta, printa, mashine ya kutolea kopi na mafaili ya kufungulia kesi.

2. Mahakama ya Ardhi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja iliyopo Gamba imeshindwa kuanza kazi kutokana na jengo lake kukosa fedha za matengenezo ili liweze kuendana na shughuli za kimahakama ambayo gharama za matengenezo hayo ni zaidi ya milioni 72.

3. Malipo ya wazee wa Mahakama ambao hulipwa posho zao kupitia OC ya Mahakama hupelekea kutumia kiwango kikubwa cha fedha hizo kwa kuwalipa wazee hao, hivyo Mahakama kushindwa kuendeleza mipango yake mengine ambayo imepanga kukamilisha kwa kila mwaka.

4. Uchakavu wa jengo la ofisi kuu ya Mahakama ya Ardhi (Majestik) ambayo pia ni Ofisi ya Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Mahakama hiyo inakabiliwa na uchakavu wa jengo lake kwa muda mrefu sasa, na fedha za gharama za matengenezo ya jengo hilo bado hazijapatikana ukizingatia kwamba jengo hilo kwa sasa linatumika pia kama ni Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja.

5. Kutofikiwa kwa malengo ya bajeti yaliopangwa katika Mahakama ya Ardhi. Hii inatokana na agizo lililotolewa na Serikali la kuwalipa Wazee wa Mahakama Shilingi 20,000 badala ya Shilingi 10,000 hali ambayo imepelekea kuathirika kwa hali ya bajeti ya Mahakama hiyo kulingana na Bajeti waliopangiwa kwa mwaka.

6. Uchakavu wa majengo ya Mahakama za Ardhi Pemba yanapelekea ofisi moja kutumiwa na watu zaidi ya mmoja. Mfano halisi, Mahakama ya Ardhi ya Wete (Pemba) ambapo ofisi moja inatumika na Hakimu, Karani, Wahudumu pamoja na Matarishi wa Mahakama.

7. Kwa upande wa jengo la Mahakama ya Mkoa wa Kusini Pemba liliopo Chake-Chake, jengo hili linakabiliwa na uhaba wa ofisi za wafanyakazi wake. Hivyo, ipo haja kufanyiwa nyongeza ya sehemu ndogo iliyopo kwenye jengo hilo.

8. Ukosefu wa usafiri, Mahakama haina gari hata moja kwa Unguja na Pemba ukizingatia miongoni mwa shughuli zinazofanywa na Mahakama ni kutembelea na kufanya ukaguzi (site visit) kwenye maeneo yenye migogoro ya ardhi mijini na mashamba.

9. Mahakama ya Ardhi inakabiliwa na upungufu wa samani kwa ajili ya wafanyakazi wake kitu ambacho kinasababisha baadhi ya wafanyakazi kufanya kazi zao kwa usumbufu mkubwa.

10. Uwasilishwaji wa nyaraka zisizo halali mbele ya Mahakama wakati wa usikilizaji kesi zinazohusu migogoro ya ardhi.

11. Uchache wa wafanyakazi wa kada mbalimbali hususan wachapaji (typists), walinzi na wahudumu.

12. Mahakama moja kufanya kazi za Mahakama mbili. Mfano halisi ni Mahakama ya 'Majestic' inafanya kazi pamoja na za Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa wakati mmoja, jambo ambalo linalopelekea kupunguza ufanisi katika usikilizaji wa kesi.

13. Ukosefu wa ushirikishwaji wa Mahakimu wa Mahakama ya Ardhi katika baadhi ya mafunzo yanayoandaliwa na Uongozi wa Mahakama.

14. Kukosekana kwa maslahi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi tangu kuteuliwa kushika wadhifa huo na Mheshimiwa Rais.

### 2.2.4.2 **MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Mahakama ya Ardhi kuwa makini wakati wote wa uamuaji wa kesi zinazohusiana na migogoro ya ardhi hususan katika muda wa kukusanya ushahidi na ukaguzi wa nyaraka.

2. Kamati inaiomba Mahakama ya Ardhi pamoja na Kamisheni ya Ardhi kufanya kazi kwa karibu ili kuweza kupunguza idadi ya migogoro ya ardhi inayozidi kuendelea siku hadi siku inayotokana na uhaulishaji unaofanywa kinyume na Sheria.

3. Kamati inaitaka Wizara kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kulitafutia ufumbuzi suala zima linalohusiana na ongezeko la asilimia 100 la malipo ya posho za Wazee wa Mahakama ya Ardhi linatokana na agizo la Serikali ambalo limeathiri utendaji mzima wa mwaka huu kwani fedha za OC zaidi ya nusu zinalipwa kwa Wazee wa Mahakama “accessors” ambapo suala hilo halikupangwa katika bajeti iliyopita.

4. Kamati inaitaka Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kuongeza idadi ya Mahakimu pamoja na watendaji wengine wa Mahakama ya Ardhi kwa upande wa Unguja na Pemba.

5. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kwa ujumla kuipatia Mahakama ya Ardhi jengo jengine la kufanyia kazi ili kunusuru afya za wafanyakazi wake kutokana na uchakavu wa jengo linalotumika hivi sasa hapo ‘Majestic’.

6. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara husika kutenga fungu maalumu la fedha katika bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya kulifanyia matengezo jengo la Mahakama ya Ardhi liliopo Gamba ili kuwarahisishia wananchi walioko katika Mkoa huu wa Kaskazini kupata huduma hiyo kwa urahisi.

7. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikalini kumpatia stahiki zake pamoja na posho Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi kama wanavyolipwa wateule wengine wa Mheshimiwa Rais kama Sheria zinavyoelekeza.

8. Kamati inaitaka Kamisheni ya Utumishi Serikalini kuharakisha upatikanaji wa watumishi katika Mahakama ya Ardhi kwani uhaba wa wafanyakazi hukwamisha utendaji wa Mahakama hizo na kucheleweshe utatuzi wa migogoro ya Ardhi pamoja na kucheleweshe utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya kumaliza migogoro ya Ardhi hapa Zanzibar.

### 2.2.5 **MRAJIS WA ARDHI**

Afisi ya Msajili/Mrajis wa Ardhi ni moja kati ya Taasisi zilizo chini ya Kamisheni ya Ardhi. Taasisi hii imeanzishwa chini ya Sheria ya Ardhi Namba 10 ya mwaka 1990. Kazi kubwa ya Taasisi hii ni kusajili ardhi na kuweka kumbukumbu za uhaulishaji wote unaofanywa katika ardhi iliyosajiliwa.

Pamoja na hayo, Kamati hadi inapokea taarifa hii imesikitishwa na utendaji kazi ya Afisi hii na hatua zinazochukuliwa katika utekelezaji wa kazi zao za usajili wa ardhi ili kusaidia kupunguza migogoro mtambuka ya ardhi inayoibuka siku hadi siku. Kwani tangu kuanzishwa kwa Afisi hii imeweza kutoa kadi 90 za usajili wa ardhi, kufanyika kwa utambuzi wa ardhi katika maeneo machache yakiwemo Jango'mbe, Matarumbeta, Jumbi na Mji Mkongwe tu hadi sasa, kufanya usajili wa ardhi za mirathi 7 kati ya 40, kutayarisha marejista 2 ya ardhi ya maeneo ya Mwembeladu na Vikokotoni pamoja na kufanikisha utayarishaji wa makala ya ardhi 12 tu.

#### 2.2.5.1 **CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI AFISI YA MSAJILI/MRAJIS WA ARDHI**

Afisi ya Mrajis wa Ardhi inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake:

1. Kukosekana kwa bajeti ya uhakika ya usajili wa ardhi, inayofanya utambuzi na usajili wa ardhi kusita.

2. Uhaba wa wafanyakazi ambapo kwa Unguja ni wafanyakazi 15 na Pemba ni 3.

3. Uelewa mdogo wa wananchi juu ya masuala mazima ya mirathi.

4. Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa Afisi ya Msajili wa Ardhi, hali inayopelekea gari ya Mkurugenzi kutumika na Mhasibu pamoja na watendaji wengine katika shughuli za utambuzi wa ardhi.

### 2.2.5.2 **MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Afisi ya Msajili wa Ardhi kufanya kazi kwa karibu na Afisi ya Wakfu na Mali ya Amana ili kuweza kusaidia upatikanaji wa haki za mirathi kwa haraka na kwa wakati.

2. Kamati inaiomba pia Afisi ya Msajili wa Ardhi kwa kushirikiana na Afisi ya Mufti kuendelea na zoezi la utoaji elimu kwa wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya Serikali na watu binafsi kuhusiana na umuhimu wa usajili wa ardhi pamoja na mirathi.

3. Kamati inaipongeza Serikali na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kupitia Afisi ya Msajili wa Ardhi kwa kupunguza ada ya usajili wa mali za mirathi kutoka asilimia 5 hadi kufikia 0.5.

4. Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Afisi ya Msajili wa Ardhi kwa kukamilisha kazi ya uandaji wa Sera ya Ardhi.

5. Kamati inaitaka Kamisheni ya Utumishi kuwapatia Afisi ya Msajili wa Ardhi watumishi wa kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

6. Kutokana na tatizo la usafiri, Kamati inaiomba Serikali kuwapatia magari ya kutosha ili kuweza kufuatilia kazi zao za usajili pamoja na utambuzi wa ardhi katika maeneo yote kwa upande wa Unguja na Pemba.

### 2.2.6 **IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI**

Idara ya Mipango Miji na Vijiji inafanyakazi ya utekelezaji wa Sheria ya Mipango Miji na Vijiji, Sura 85 ya 1995. Lengo kuu la Idara hii ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inajiwekea mipango mizuri na endelevu ya matumizi na maendeleo ya ardhi na kusimamia utekelezaji wake. Pia, kwa kupitia Kanuni za Sheria ya Mipango Miji na Vijiji ya mwaka 2015 iliyoanzisha Kamati ya Usimamizi na

Udhibiti wa Ujenzi kupitia Kamisheni ya Ardhi, Idara hii hufanyakazi kwa kushirikiana na Manispaa, Halmashauri, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, Mamlaka ya Usimamizi wa Manzingira (ZEMA), Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo pamoja na Bodi ya Wakandarasi.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati haijafurahishwa na utendaji wa idara hii hasa kwa upande wa Pemba ambapo hadi kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Kamati, hakuna utekelezaji uliofanyika kwa upande wa utoaji vibali ndani ya Mji wa Pemba ili kupunguza ujenzi holela, uvamizi wa maeneo ya wazi na migogoro ya ardhi.

#### 2.2.6.1 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI

Idara ya Mipango Miji na Vijiji inakabiliwa na changamoto zifuatazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yake:

1. Ufinyu wa Bajeti jambo unaopelekea kazi zinazopangwa kushindwa kutekelezwa kwa wakati. Hii inatokana na kutegemea OC moja inayoingiziwa Kamisheni ya Ardhi igawanywe katika idara zote nne zilizo chini yake ambapo ni wazi kuwa haitoshi.

2. Uhaba wa wataalamu katika idara hii hali inayosababisha kuzorota kwa majukumu pamoja na shughuli za upangaji miji katika Miji na Vijiji.

3. Ucheleweshwaji wa uingizwaji wa OC kutoka Serikalini.

4. Kukosekana kwa mashirikiano baina ya Idara na Taasisi za Tawala za Mikoa hususan katika miradi mikubwa yenye tija na manufaa kwa wananchi na nchi kwa ujumla.

### 2.2.6.2 **MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaiomba Wizara kupitia Idara ya Mipango Miji na Vijiji kuandaa mafunzo maalum kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi juu ya suala nzima la utiaji thamani ardhi ya Zanzibar.

2. Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kulitafutia ufumbuzi mbadala tatizo la ucheleweshwaji wa uingizwaji wa OC katika Wizara zote za Serikali pamoja na Taasisi zake. Katika kulipatia ufumbuzi suala hili ni vyema kila idara kuwa na fungu lake la matumizi. Kutokufanya hivyo kunapelekea kazi nyingi kushindwa kutekelezeka.

3. Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara husika kuwapa kipaumbele watendaji wa idara hii hasa pale inapotokezea uwekezaji wa miradi mikubwa ndani ya nchi. Kwa mfano, Ujenzi unaoendelea huko Fumba na Nyamanzi.

4. Kamati inaiomba Serikali kupitia Idara hii kutafuta maeneo ya kuweza kujenga kumbi za kisasa kwa ajili ya mikutano na shughuli za Serikali.

5. Kutokana na kuongezeka kwa ujenzi wa skuli katika eneo lililotengwa na Serikali kwa ajili ya Mradi wa makaazi katika eneo Mwembeshauri, Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Idara ya Mipango Miji kujenga njia za juu za wanaoenda kwa miguu “flyover” katika eneo linalojengwa Skuli ya Sekondari ya Rahaleo ili kunusuru watoto wetu hasa kwa kuzingatia kuwa kituo kikuu cha Magari kinajengwa hapo kichangwani.

6. Idara hii haina usafiri wa ndani jambo linalopekea watendaji kutumia magari yao katika shughuli za Serikali jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada zao za kazi. Kutokana na kadhia

hiyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha watendaji wanapatiwa usafiri ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

## 2.3 **SEKTA YA MAJI**

### 2.3.1 **MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)**

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeanzishwa chini ya Sheria ya Maji, Namba 4 ya Mwaka 2006 kama ilivyopendekezwa katika Sera ya Maji ya Taifa ya Zanzibar ya mwaka 2004, ikiwa na jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kulinda na kuhifadhi rasilimali maji.

Kamati hadi inapokea taarifa hii bado kuna baadhi ya miradi ambayo utekelezaji wake unasuasua na hatimae kupelekea wananchi kuvunjika moyo. Miongoni mwa miradi hiyo:

(a) Mradi wa Uchimbaji Visima unaofadhiliwa na Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa China.

(b) Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira wa Mkoa wa Mjini Magharibi – ADF 12.

(c) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji ya Mkoa wa Mjini - JICA.

(d) Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar – Exim Bank, India.

(e) Mradi wa utekelezaji wa Uchimbaji wa Visima vya Ras Al Khaimah.

Hata hivyo, hatua mbalimbali za uendeshaji wa visima hivyo kwa kazi za upelekaji umeme, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu na ulazaji mabomba makubwa na madogo kwa juhudi za Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) zimeanza na zinaendelea vizuri. Hadi kufikia tarehe 15 Januari 2018, idadi ya visima ambavyo tayari vimeendelezwa na kuanza kutoa huduma kikamilifu na

idadi ya visima vyengine vinavyoendelezwa ni kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli lifuatalo:

**Mwenenndo wa Uendelezaji Visima vilivyochimbwa na Mradi wa Uchimbaji Visima Zanzibar – Ras Al Khaimah**

| Mkoa | Vilivyochimbwa | Vinavyotoa huduma | Vinavyoendelezwa | vilivyosalia |
|---|---|---|---|---|
| Mjini Magharibi | 49 | 4 | 10 | 35 |
| Kaskazini – (u) | 29 | 3 | 3 | 23 |
| Kusini – (U) | 35 | 4 | 3 | 28 |
| Kaskazini – (P) | 14 | 8 | 1 | 5 |
| Kusini – (P) | 23 | 10 | 6 | 7 |
| **Jumla** | **150** | **29** | **23** | **98** |

### 2.3.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA MAJI (ZAWA)

1. Ucheleweshwaji wa ulipaji fidia kwa wananchi katika maeneo ya miradi ilipotekelezwa.

2. Uchakavu wa miundombinu ya maji Unguja na Pemba.

3. Ufinyu wa Bajeti  inayopelekea kazi za Mamlaka kusuasua.

4. Muitikio mdogo wa wananchi juu ya uchangiaji wa huduma ya maji kwa hiari.

5. Uvamizi wa viazio vya maji vinavopunguza kwa kasi rasilimali ya maji.

6. Kuchelewa kwa Mradi wa Maji unaofadhiliwa na Exim Bank mpaka wananchi kuanza kuuliza kulikoni mpaka leo hakuna kilichofanyika.

7. Kuchelewa kuunganishwa na mitandao ya maji kwa Visima vya Ras El Khaimah ni moja wapo wa sababu iliyopelekea ukosefu mkubwa wa maji katika maeneo ya Mjini na Vijijini.

8. Kuungua kwa “pump” nyingi katika visima kumesababisha visima vingi kuwa na uhaba wa maji.

9. Uchakavu wa Karakana ya Mamlaka ya Maji iliopo Saateni pamoja na uhaba wa wataalamu ni miongoni mwa changamoto inayowakabili Mamlaka.

### 2.3.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kutoa elimu kwa wananchi juu ya suala zima la uchelewaji wa utekelezaji wa Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar unaofadhiliwa na “Exim Bank” ya India pamoja na Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji ya Mkoa wa Mjini unaofadhiliwa na “JICA”.

2. Kamati inaitaka Serikali kuharakisha ulipaji wa fidia za wananchi ambao aidha mazao au ardhi zao ziliathirika katika utekelezaji wa Shughuli za uwekaji miundombinu ya maji.

3. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka husika kuandaa mpango mkakati wa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watendaji wake wa ndani.

4. Kamati inaitaka Mamlaka ya Maji kuharakisha ufungaji wa Mita za maji kwa wananchi ili kuondokana na changamoto ya upotevu wa maji.

5. Kutokana na tatizo la uvamizi wa vianzio vya maji, Kamati yangu inaishauri Serikali kuanzisha Mamlaka ya Uhifadhi wa Mabonde na Vianzio vya Maji hapa Zanzibar ili kuhakikisha uvamizi na uharibifu wa vianzio vya maji unadhibitiwa.

6. Kamati pia inaiomba Serikali pamoja na Wizara husika kuunda chombo chengine kwa ajili ya kusambaza huduma ya maji na kuiachia Mamlaka kazi ya kubuni na kupanga miradi mikubwa pamoja na masuala ya kiutawala tu ili kuleta ufanisi wa upatikanaji wa huduma hii hapa Zanzibar.

7. Kamati inaitaka Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuharakisha zoezi la kuviunganisha Visima vilivyochimbwa na Raas El Khaima kama agizo la Serikali linavyoelekeza.

## 2.4 **SEKTA YA NISHATI**

### 2.4.1 **SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)**

Shirika la Umeme Zanzibar miongoni mwa majukumu yake makubwa ni kuhakikisha kuwa huduma ya umeme inapatikana wakati wote katika hali ya ubora na usalama. Hivyo, ili kufikia lengo hilo inalazimu kuhakikisha kuwa vituo vya kupokelea, kupoozea na kudhibiti umeme vya Ras Kiromoni, Fumba, Mtoni, Mpendae, Mwanyanya na Welezo vinaendea vizuri. Lengo hilo limefikiwa ambapo vituo vyote vinafanya kazi vizuri.

Aidha, kiwango cha juu cha matumizi ya umeme kilichofikiwa kwa upande wa Unguja ni Megawati sitini na nane (68. 4MW) katika kipindi hicho cha robo mwaka iliyoishia tarehe 30 Disemba, 2017.

Kwa upande wa Unguja Madeni ya Wateja wa Umeme Oktoba hadi Disemba, 2017 ni kama yanayoonekana katika jadweli lifuatalo:

| **NAM.** | **JINA LA TAASISI** | **DENI LILOBAKIA ( MEI – DISEMBA) 2017** |
|---|---|---|
| *1.* | ZAWA | 12,284,855,078.46 |
| *2.* | TAASISI NYENGINE ZA SMZ | 1,531,117,363.33 |
| *3.* | TAASISI ZA SMT | 1,527,747,667.28 |
| | **JUMLA YA DENI LA SMZ NA SMT** | **15,343,720,109.07** |

Pamoja na madeni sugu yanayoikabili Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), bado Shirika la Umeme kwa miaka ya hivi karibuni limekua likifanya vizuri sana kwa upande wa Unguja na Pemba, ambapo umeme umekuwa ukisambazwa karibu katika Wilaya zote za Unguja na Pemba hadi katika Visiwa vidogo vidogo. Shirika limekuwa likiongeza ukusanyaji wa mapato yake siku hadi siku na pia limejitahidi kwa kiasi kikubwa kudhibiti vitendo vya ubadhirifu katika shirika pamoja na kudhibiti vitendo vya wizi wa umeme jambo ambalo Kamati yangu imeridhika sana na kwa mara ya kwanza Shirika hivi sasa limeanza kulipa gawio Serikalini. Kutokana na mafanikio hayo, Kamati yangu inalipongeza Shirika kwa kazi hiyo nzuri.

**TAWI LA PEMBA**

Tawi la Pemba pia lina jukumu la kusimamia utendaji kazi kwa vitengo vyote vya Shirika la Umeme vilivyoko Pemba.

Katika kipindi cha robo ya kwanza Julai - Septemba, 2017 upatikanaji wa umeme ulikuwa ni wa kuridhisha, hata hivyo, ‘line’ ya Pemba -Tanga ilikosa umeme mara 8 kwa jumla ya dakika 46, matumizi makubwa zaidi ya umeme kwa kipindi hiki yalifikia 8.01 MVA (7.7 MW) mnamo tarehe 31 Agosti, 2017 na hadi kufikia mwezi Septemba, 2017 watumiaji wa huduma ya umeme walifikia 30,003 kati ya hao watumiaji 25,276 wanatumia mita za TUKUZA.

Kwa upande wa Pemba madeni makubwa ya baadhi ya taasisi za Serikali hadi kufikia Disemba, 2017 ni kama yanavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

| NAM. | JINA LA TAASISI | DENI LILOBAKIA ( MEI – DISEMBA) 2017 |
|---|---|---|
| *1.* | ZAWA | 1,721,380,318.39 |
| *2.* | WIZARA YA AFYA | 73,969,528.53 |
| *3.* | TAASISI NYENGINE ZA SMZ | 2,678,975,389.66 |
| | **JUMLA KUU** | **4,474,325,236.58** |

### 2.2.6.3 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA UMEME KWA UNGUJA NA PEMBA

1. Ukosefu wa huduma ya umeme katika baadhi ya vijiji katika kisiwa cha Pemba. Mfano mzuri Shehia ya Sizizini.

2. Ongezeko kubwa la madeni kwa upande wa Shirika la Umeme yanayotokana na baadhi ya Taasisi za SMZ, SMT pamoja na wateja binafsi kwa upande wa Unguja na Pemba.

3. Ukosefu wa mita za Tukuza umepelekea watu wengi kukosa huduma ya umeme kwa wakati.

4. Uhaba wa bajeti hususan za upelekaji umeme visiwani kama vile kisiwa cha Kokota, Fundo na Mtambile.

5. Uchakavu wa nguzo za umeme hali inayopelekea wananchi kukosa huduma muhinu ya umeme katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba.

### 2.2.6.4 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati pia inaipongeza Serikali pamoja na Shirika la Umeme kwa kufanikisha kuendelea na ulipaji wa deni la Umeme Tanesco ambapo hadi kufikia mwezi Disemba jumla ya Tshs. Bilioni 29.8 zimeshalipwa.

2. Kamati inaipongeza Serikali pamoja na Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa kufanikisha upelekaji wa huduma ya umeme katika vijiji vya Wingwi/Kinazini na Fundo kwa upande wa Pemba.

3. Kamati inaipongeza Wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa kufikia lengo na shabaha za kuhakikisha huduma ya umeme inawafikia wananchi wa mijini na vijijini katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

4. Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikana na Wizara husika kuharakisha ulipaji wa madeni yanayotokana na baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo hadi kufikia mwezi wa Disemba Shirika linadai Tshs, Bilioni 15,343,720,109.07.

5. Kamati inaishauri Wizara pamoja na Shirika husika kuwaongezea ujuzi wataalamu wao wa ndani katika kada tofauti kwa manufaa ya kuliendesha Shirika Kibiashara na sio kutoa huduma.

6. Vile vile, Kamati inasikitishwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutolitekeleza ipasavyo agizo la Kamati la ukataji wa 'OC' za kila taasisi ya Serikali zinazodaiwa na Shirika la Umeme ili kulipa nguvu Shirika kuweza kujiendesha.

7. Kamati yangu inaitaka Serikali kwa hivi sasa kubeba mzigo wa kulilipa deni la Mamlaka ya Maji hadi hapo watakapoweza kujilipia wenyewe kwani kila siku linaongezeka na kulipa mzigo mkubwa Shirika la Umeme jambo ambalo linarejesha nyuma jitihada zao za kujitegemea.

8. Kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu deni la ZECO kwa TANESCO, fedha hizo kulipwa ZECO na wao ndio walipe TANESCO kwasababu inayodaiwa ni ZECO na sio Wizara ya Fedha na Mipango.

9. Kamati yangu pia inaunga mkono hatua zilizoanza kuchukuliwa na Shirika la Umeme la kuvifungia Mita za Tukuza baadhi ya Visima vya Maji ili Mamlaka ya Maji (Zawa) iweze kubuni mbinu mbadala za kuongeza ukusanyaji

wa mapato pamoja na kumudu kulipa madeni ya Umeme yanayotokana na Visima vyao vya usambazaji wa Maji mijini na Vijijini.

### 2.4.2 MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) ni Taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya mwaka 2016 ya Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia. Mamlaka hii ina jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

Aidha, Kamati katika ziara zake ilikumbushia Mamlaka kuzingatia mambo yote ya msingi yaliotajwa katika Sheria hii ambayo ni muhimu kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Miongoni mwa mambo hayo ni umiliki wa rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia katika eneo la Zanzibar ni mali ya watu wa Zanzibar, Kuanzishwa kwa Taasisi za Usimamizi wa rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia, Utaratibu wa utafutaji na uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na Ukomo wake, Masuala ya afya, usalama na uhifadhi wa mazigira, thamani ya wadau wa ndani na ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na Kuanzishwa Mfuko wa mapato na matumizi yanayotokana na uzwaji wa rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia.

### 2.2.6.5 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA UDHIBITI WAUTAFUATAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA)

1. Ucheleweshwaji wa ajira za wataalamu wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

2. Matarajio makubwa kwa wananchi katika upatikanaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

3. Uelewa mdogo wa wananchi katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

4. Kukosekana sehemu ya kisasa pamoja na vifaa vya kuhifadhi, kuchakata na kuzitumia taarifa za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.

5. Kuchelewa kuundwa kwa Kampuni ya Petroli Zanzibar “ZPDC” pamoja na uchelewaji wa kuundwa kwa Bodi ya Mamlaka ya utafiti na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar

## 2.2.6.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuwashirikisha kikamilifu wananchi wa maeneo husika pindi tafiti zinapokuwa zinafanywa katika maeneo ya baharini pamoja na nchi kavu ili nao waweze kufaidika na matunda ya uwekezaji huo.

2. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara kuharakisha uundwaji wa Kampuni ya Mafuta ya Serikali ili kuweza kutimiza masharti ya Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa rasilimali ya Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

3. Kamati inaipongeza Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa kuendelea na mpango wa kutoa elimu mijini na vijijini kwa upande wa Unguja na Pemba.

4. Kamati pia inaitaka Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuwapatia vijana wenye taaluma ya masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ili waanze kupata uzoefu kwa kuwa hivi sasa wapo wa kutosha ili waanze kazi na pia kuwapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili mara tu tutakapoanza shughuli za uzalishaji wa Mafuta na Gesi basi tuweze kuwatumia wataalamu wetu wa ndani.

### 2.4.3 MAMLAKA YA UDHIBITI YA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) ni taasisi iliyoundwa kwa Sheria Namba 7 ya mwaka 2013 ambapo jukumu lake kubwa ni kusimamia upatikanaji wa huduma bora za maji na nishati kwa wananchi.

Aidha, hadi Kamati inapokea taarifa hii jumla ya lita 35,472,351 za mafuta zimeingizwa nchini kwa kutumia mfumo wa ununuaji wa mafuta kwa pamoja (BPS) kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2017.

#### 2.4.3.1 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)

1. **Hali ya Bandari ya Mtoni:** Kutokana na hali ya bandari ya Mtoni, utekelezaji wa mfumo wa (BPS) uliathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na kina cha maji katika eneo hilo kutokidhi haja ya kufunga gati kwa meli kubwa. Kwani kama inavyoeleweka uwezo wa bandari ya Mtoni ni kwa meli zisizozidi tani (3,500) na kwa upande wa Pemba ni meli zisizozidi tani (600).

2. **Bohari ya Kuhifadhia Mafuta:** Kukosekana kwa bohari kubwa ambayo itawezesha muagizaji na muingizaji wa mafuta kuweza kuhifadhi mafuta yake baada ya kufika Zanzibar, hali hii inapelekea upungufu wa mafuta mara kwa mara.

3. **Ufunguzi wa Hati ya Malipo:** Baadhi ya kampuni za mafuta (OMCS) kushindwa kufungua hati za malipo (letter of credit) kwa wakati kulipelekea kuchelewa kushushwa na kusambazwa kwa mafuta nchini.

4. **Gharama ya Uletaji wa Mafuta Zanzibar:** Hii ilitokana na changamoto za uingizaji mafuta Zanzibar, ikijumuisha miundombinu hafifu ya bandari ya Mtoni.

5. **Ongezeko la mafuta ya magendo kwa upande wa Pemba:** Hali inayopelekea kusambaa kwa kiwango kikubwa kwa mafuta yaliyochakachuliwa.

6. **Ongezeko la bei ya mafuta:** Jambo ambalo linatokana na gharama za usafirishaji kuwa kubwa tofauti na mategemeo ya wananchi.

7. **Ucheleweshaji wa Meli ya Mafuta:** Hii inatokana na mletaji mafuta kuchelewa kuleta mafuta kwa wakati na kusababisha upungufu wa mafuta mara kwa mara na hatimae kuzorotesha shughuli za kijamii na kiuchumi.

8. **Uwezo Mdogo wa Mkampuni ya Mafuta:** Kubainika kwa baadhi ya kampuni za mafuta kutokuwa na uwezo wa kununua mafuta yalioingizwa kwa mfumo wa BPS na wakati mwengine kupunguza kiwango cha uingizwaji. Hali hii imekua ikichangia kuanza kuonekana kwa foleni katika baadhi ya Vituo vya mafuta.

### 2.4.3.2 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kufanya kazi kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama ili kuweza kupunguza tatizo la usafirishaji wa mafuta ya magendo katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

2. Kamati inaiomba Serikali kukaa pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kuandaa mpango mkakati juu ya matumizi ya eneo la Mwangapwani lililotengwa kwa ajili ya shughuli za Mafuta.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuweka miundombinu mbadala kwa ajili ya uingizaji mafuta ndani ya nchi katika Bandari yetu ya Zanzibar.

4. Kamati inaitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kuendelea na utoaji wa elimu kwa jamii juu ya athari za uuzaji wa mafuta ya magendo na uchakachuaji.

5. Kamati inaiagiza Bodi ya ZURA kushirikiana na Bodi ya Wakandarasi wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa jengo la ofisi za ZURA unaotarajiwa kuanza mwezi wa Februari.

6. Kamati inashauri kuwekwe bomba moja tu la Serikali la kupitishia Mafuta yanayoteremshwa na yanayopakiwa ili kuweza kuweka takwimu sahihi kwa Mafuta yatakayoingia Nchini na yatakayosafirishwa ambapo umiliki wa bomba hilo uwe chini ya Serikali ili kudhibiti mapato ya Nchi.

7. Kamati inashauri Miundombinu itakayowekwa huko Mangapwani iwe ni ya aina mbili moja iwe kwa matumizi ya hapa nchini na mingine iwe ni ‘Storage’ ya kusafirisha Nchi nyingine yaani “Transit” ili kuongeza wigo mpana wa mapato Nchini kwetu.

## 2.5 **SEKTA YA MAZINGIRA**

### 2.5.1 **MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR (ZEMA) NA IDARA YA MAZINGIRA ZANZIBAR**

Mamlaka ya Usimamizi na Idara ya Mazingira Zanzibar pamoja na mambo mengine ina jukumu la kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango vya Mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafu na uharibifu.

Sambamba na hilo, Mamlaka imefanya operesheni za kusimamia marufuku ya mifuko ya plastiki, kufanya Operesheni za kusimamia maliasili zisizorejesheka Unguja na Pemba, kufanya ziara za ufuatiliaji wa kimazingira, kusimamia Tathmini za Kimazingira kwa miradi, kufanya ziara ufuatiliaji wa miradi ya kiuchumi na kimaendeleo, kukuza uelewa na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira, kuimarisha utendaji wa Ofisi na kushiriki warsha pamoja na mikutano ya ndani na nje.

Aidha, Kamati katika kupokea taarifa ilifurahishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) ambayo katika robo ya pili (Oktoba - Disemba, 2017) imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 15,300,000/= sawa na wastani wa asilimia 142 ya kiwango kilichopangwa kukusanywa.

### 2.5.1.1 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR NA IDARA YA MAZINGIRA

1. Ufinyu wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Mkurugenzi wa Idara ya Mazingira kwa upande wa Unguja na Pemba wanafanya kazi katika Ofisi moja hali inayopelekea kukosekana kwa faragha za kiutendaji.

2. Umwagaji wa maji taka katika eneo la Maruhubi unaathiri utendaji kazi kwa wafanyakazi kutokana na kuchafuka kwa hali ya hewa eneo la karibu na Ofisi.

3. Sheria ya Mazingira ya Zanzibar inatofautiana na Sheria ya Tanzania Bara katika masuala ya kuzuia mifuko ya plastiki. Hali inayoweza kupelekea uingizwaji wa bidhaa hiyo kirahisi Zanziabar.

4. Utupaji ovyo taka katika maeneo ya Mjini na Vijijini.

5. Umwagaji ovyo wa maji machafu yanayotapishwa kwenye vyoo na makaro katika eneo la Maruhubi Zanzibar.

6. Uchimbaji ovyo wa mchanga kwenye maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Hali hii inasababisha athari kubwa za mmong’onyoko wa ardhi katika maeneo mengi visiwani mwetu.

7. Baadhi ya miradi ya Ujenzi kutofuata taratibu za kimazingira.

### 2.5.1.2 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Serikali pamoja na Wizara kwa jitihada zake za kuelimisha wananchi juu ya utumiaji mzuri wa mazingira kupitia Redio na TV. Aidha, Kamati inashauri kutokana na jitihada hizo pia kushirikiana na masheha kuendelea kutoa elimu hiyo ya ana kwa ana katika miji na vijiji.

2. Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara kuiangalia Sheria upya kwa upande wa wanaoingiza mifuko ya plastiki pamoja na wanaokamatwa nayo wakati wa matumizi, pamoja na kuandaa kanuni za kulipa faini za papo kwa hapo.

3. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kukaa na Halmashauri zote kuandaa kampeni za kuwashajihisha wananchi kutengeza mazingira ya Zanzibar katika hali ya usafi. Sambamba na zoezi la upandaji miti liwe endelevu pamoja na kuandaa vitalu kwa ajili ya kupata miti hiyo.

4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kutafuta vianzio vya kuendeleza mazingira kifedha kwa kuhifadhi, kudhibiti na kuendeleza mazingira katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

5. Kamati inaitaka Serikali pamoja na Wizara kuwapeleka watendaji nchini Rwanda kupata elimu ya kuhifadhi maji machafu kwa kuyarudisha tena katika hali ya kuweza kutumika kwa manufa ya vizazi vijavyo na Taifa kwa ujumla.

6. Kamati inaagiza Mamlaka na Idara ya Mazingira kufanya mpango mkakati maalumu dhidi ya mtaro ambao umepita Saateni unaojengwa kwa kuinua kuta na kusababisha maji kuingia mpaka katika nyumba za watu pamoja na kufanya ziara katika sehemu hiyo.

7. Kamati inazitaka taasisi zote za Serikali na za watu binafsi kabla ya kuanzisha miradi yao mikubwa kwanza kupitia Idara ya Mazingira ili kupata miongozo na taratibu za kuhifadhi na kulinda kimazingira ili hapo baadae isilete uharibifu wa Mazingira.

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

### 2.6 UTANGULIZI

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji imepewa majukumu makuu ya kusimamia Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar. Kwa mwaka wa 2017/2018, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (Vission 2020), MKUZA III, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020, Sera ya Usafiri Zanzibar (2008), Sera ya TEHAMA, Sera ya Taifa ya Nyumba, na Mpango Mkuu wa Usafiri (Zanzibar Transport Master Plan, 2009) kwa kufuata Bajeti inayotumia programu (PBB).

Taasisi zinazosimamiwa na Wizara zinatekelezwa kupitia Idara, Mashirika na Mamlaka zifuatazo:

(i) Ofisi Kuu, Pemba.
(ii) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
(iii) Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
(iv) Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.
(v) Idara ya Usafiri na Leseni.
(vi) Idara ya Mawasiliano.
(vii) Mamlaka ya Usafiri wa Baharini.
(viii) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.
(ix) Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.
(x) Shirika la Meli na Uwakala.
(xi) Shirika la Bandari.
(xii) Shirika la Nyumba.
(xiii) Wakala wa Majengo.

Katika ripoti hii, Kamati inaigawa Wizara hii katika Sekta za Utawala, Sekta ya Nyumba, Usafiri wa nchi kavu, Usafiri wa Anga, Usafiri wa Majini na Mawasiliano.

### 2.6.1 **SEKTA YA UTAWALA**

Sekta hii inaundwa na Ofisi Kuu Pemba, Idara ya Mipango na Utumishi na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Jukumu kubwa la Sekta hii ni kusimamia masuala ya kiutumishi, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa upande wa Unguja na Pemba.

Aidha, sekta hii pia inaratibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kupitia programu zake nne kama ifuatavyo:

(a) Programu ya Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabara.
(b) Program ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe na Uimarishaji wa Majengo ya Serikali na Binafsi.
(c) Program ya Huduma za Technolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).
(d) Program ya Mipango na Utawala katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

#### 2.6.1.1 **CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA UTAWALA**

1. Kukosekana kwa mawasiliano mazuri baina ya Idara ya Mawasiliano na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara wakati wa Ujenzi wa Barabara na wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Mkongo wa Taifa jambo ambalo limepelekea Mkongo huo kuathirika kwa kukatwa na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali.

2. Bodi karibu tatu katika Wizara hii zimekwisha muda wake bila ya kuteuliwa wajumbe wengine hali inayosababisha Wenyeviti wa Bodi hizo kukaa bila ya kufanya kazi wanazopaswa kuzifanya kwa mujibu wa Sheria.

### 2.6.1.2 **MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara katika utekelezaji wa miradi mikubwa inayokusudiwa kutekelezwa baina ya Serikali yetu na Wafadhili kutoka nje kwa lengo la kuleta maendeleo katika Taifa letu kabla ya kuanza kutekelezwa miradi hiyo ifanyike tathmini ya kina kwa mradi yote ili kuondokana na hasara za baadae.

2. Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuharakisha ununuzi wa Mtambo wa kutengenezea lami. Mtambo uliopo sasa ni wa muda mrefu na kupelekea kushindwa kufanya kazi kwa wakati uliopangwa na hatimae kupelekea kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi na kupelekea Serikali kuingia katika hasara kubwa.

3. Kamati inaitaka Wizara kwa kushirikiana na Serikali kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Mageuzi ya Idara ya Utunzaji na Uendelezaji wa Barabara (UUB) kwa kuleta Mswada wa Sheria ambao utaanzisha Mamlaka hiyo kama ilivyo kwa wenzetu Tanzania Bara.

4. Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara kuharakisha ununuzi wa meli mpya ya abiria na mizigo na hatimae kuiuza meli ya MV. Mapinduzi II, Meli ambayo uendeshaji wake umekuwa ni wenye kuitia hasara Serikali.

5. Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kukamilisha matengenezo ya Barabara ya Michenzani – Kisonge na Saateni – Kinazini.

6. Kamati inaitaka Serikali kupitia Waziri kuteua Wajumbe wa Bodi tatu zilizomo kwenye Wizara hii ili kuwafanya wakurugenzi kufanya kazi zao ipasavyo ambazo mpaka Kamati inapokea taarifa hii zilikuwa hazijapata wajumbe.

7. Kamati inaiomba Serikali kupitia Idara ya Mipango kuweka taa za Barabarani kwenye Barabara ya Amani - Mtoni kwani hivi sasa imekuwa Barabara kubwa inayotumiwa na magari mengi ikiwemo watalii wanaoelekea Mkoa wa Kaskazini Unguja.

8. Kamati yangu inaishauri Serikali kuhakikisha katika Ujenzi wa Barabara za mjini kujengwa sambamba na njia za wapitao kwa miguu ili kuongeza ubora na usalama. Hii iende sambamba na kila kwenye makaazi ya watu basi kuwekwe njia na alama za watumiao baiskeli na wenye mahitaji maaalum (watu wenye ulemavu).

9. Kamati inaiunga mkono Wizara kwa hatua wanazochukua katika ununuzi wa mitambo ya kujengea Barabara isipokua Kamati inaitaka Idara ya Mipango ya Wizara kuwa makini katika ununuzi wa mitambo hiyo pamoja na kununua mitambo yenye kiwango bora kwa manuufa ya baadae.

### 2.6.2 **SEKTA YA NYUMBA**

Sekta hii imeundwa na Shirika la Nyumba, Wakala wa Majengo na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

#### 2.6.2.1 **SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR**

Shirika la Nyumba la Zanzibar ni taasisi inayojitegemea ambayo inafanyakazi zake kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya mwaka 2014. Sheria hii inaipa mamlaka Shirika la Nyumba la Zanzibar kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu ujenzi, uuzaji na ukodishaji nyumba za kuishi na za biashara.

Aidha, Shirika la Nyumba kwa mwaka 2017/2018, lilijipangia kutekeleza malengo mbalimbali kama vile kufanya matengenezo ya majengo ya Shirika, kuzitambua, kuzithamini na kuziorodhesha nyumba za Shirika, kukuza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi wa Shirika pamoja na kutayarisha mifumo na miongozo ya kazi.

Sambamba na hilo, Kamati pia ilibahatika kufanya ziara za kuzikangua nyumba za Serikali zinazosimamiwa na Shirika, ikiwemo nyumba za Kilimani pamoja na nyumba za Mombasa (Unguja) pamoja na kupokea taarifa ya idadi hali ya nyumba zote za Serikali kwa upande wa Unguja idadi ya nyumba hizo ni:

| NAM. | ENEO ILIPO NYUMBA | IDADI YA NYUMBA |
|---|---|---|
| *1.* | Michenzani | 723 |
| *2.* | Gamba | 138 |
| *3.* | Makunduchi | 96 |
| *4.* | Mpapa/Bambi | 70 |
| *5.* | Kikwajuni | 100 |
| *6.* | Kilimani | 13 |
| *7.* | Mombasa “A” | 61 |
| *8.* | Mombasa “B” | 29 |
| *9.* | Saateni | 30 |
| *10.* | Beit ras | 2 |
| *11.* | Mji Mkongwe | 320 |
| **Jumla** | | **1,582** |

Kwa upande wa Pemba idadi ya nyumba hizo ni:

| NAM. | ENEO ILIPO NYUMBA | IDADI YA NYUMBA |
|---|---|---|
| *1.* | Madungu | 48 |
| *2.* | Machomanne | 37 |
| *3.* | Mtemani | 105 |
| *4.* | Micheweni | 38 |
| *5.* | Mkoa/Mapinda | 43 |
| *6.* | Mkoa/Nga’mbu | 2 |
| *7.* | Kengeja | 2 |
| **Jumla** | | **275** |

### 2.6.2.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR

1. Hadi sasa Shirika halijafanikiwa kupata hata kiwanja kimoja kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Shirika licha ya maombi wanayofanya.

2. Uchakavu wa jengo la ofisi la Shirika la Nyumba.

3. Kodi ya VAT katika gharama za ujenzi na matengenezo ya majengo ya Shirika.

4. Kwa kuwa huduma za Shirika zinalipwa kupitia benki moja kwa moja, ukusanyaji wa mapato unapungua kutokana na usumbufu wanaopata wateja.

5. Upungufu wa wataalamu katika kada mbalimbali katika Shirika.

6. Kukosekana kwa mashirikiano baina ya taasisi za Serikali.

### 2.6.2.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kuwapatia maeneo ya kujenga Ofisi Shirika la Nyumba kwa upande wa Unguja na Pemba.

2. Kamati pia inaipongeza Wizara kupitia Shirika la Nyumba kwa kuanza kufanya matengenezo kwa baadhi ya nyumba kwa upande wa Pemba katika eneo la Madungu, Mtemani na Mkoani ili kuzihami na kuzienzi nyumba hizo.

3. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikana na Shirika la Nyumba kuweza kutafuta mbinu mbadala za kuwaongezea ujuzi watendaji wa ndani wa Shirika ili kuweza kupinga hatua katika malengo waliojipangia kuyatekeleza.

4. Kamati inalitaka Shirika kuyafanyia tathmini na uhakiki majengo yote ya Serikali yaliopo katika eneo la Mji Mkongwe ili kuweza kuzitambua na kupatikana kwa idadi halisi ya nyumba hizo.

5. Kamati inaiomba Wizara kupitia Shirika la Nyumba kuendelea kutoa elimu ya walipa kodi kupitia katika vyombo vya habari vya Serikali na watu binafsi.

6. Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kuliondolea Shirika ulipaji wa "VAT" katika majengo yake ili kuweza kulisaidia Shirika hilo kuweza kukuza mtaji wake wa ndani na hatimae kuweza kujiendesha wenyewe kama Sheria inavyoelekeza.

7. Kamati inaendelea kuishauri Serikali pamoja na Wizara kulikodisha jengo la Shirika la Nyumba kwa wawekezaji wa nje ili kuisaidia kupatikana kwa fedha ambazo zitawasaidia kujenga jengo lao la Ofisi linaloendana na hadhi na jina la ofisi hiyo.

8. Pia, Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Shirika kuanza kuzifanyia ukarabati nyumba za Serikali kwa upande wa Unguja. Miongoni mwa nyumba hizo ni Michenzani, Makunduchi, Gamba, Mpapa/Bambi, Kikwajuni, Kilimani, Mombasa "A", Mombasa "B", Saateni, Betras pamoja na Mji Mkongwe.

9. Kamati yangu inaitaka Serikali kuipatia fedha kwa wakati Shirika kwa upande wa Pemba kwani kazi ya Ukarabati huwa inashindwa kuendelea kutokana na ukosefu wa fedha. Lakini pia Kamati inatoa pongezi maalum kwa Afisa Mdhamini wa Shirika la Nyumba Pemba, Mhandisi Suleiman kwa Ubunifu wake wa kuzikarabati nyumba hizo za kihistoria ambapo zimeanza kurudi katika ubora wake.

### 2.6.2.4 WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

Wakala wa Majengo imeanzishwa kwa ‘Legal Notice’ No. 50 ya mwezi Mei, 2017 na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 12 Mei, 2017 kabla ya hapo ilikuwa ikijulikana kama Idara ya Ujenzi ambayo ilipewa jukumu kuu la kusimamia ujenzi wa nyumba za maendeleo.

Sambamba na hilo, malengo makuu ya Wakala wa Majengo ni kuwapatia viongozi na watendaji wakuu wa Serikali makaazi ya uhakika, bora na salama, kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa ujenzi wa majengo ya Serikali kulingana na mahitaji husika, kutayarisha utaratibu endelevu wa matengenezo ya majengo ya Serikali, kuweka mpango mzuri wa kuhakiki makadirio ya ujenzi katika miradi ya Serikali pamoja na kusimamia na kuendeleza majengo yote ya Serikali ikiwa ya makaazi, biashara au ofisi.

### 2.6.2.5 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

1. Wakala wa Majengo bado haijapatiwa ofisi ya uhakika kwa ajili ya kufanya kazi za kila siku, kwani hivi sasa wameanzimwa jengo la ZSSF liliopo Kilimani na hadi Kamati inapokea taarifa hii wakala imeshapokea barua kutoka ZSSF yakuwata wahame katika jengo hilo.

2. Wakala wa Majengo ina upungufu wa mashine za kisasa za kufanyia kazi katika kiwanda chake kilichopo Saateni kwani mashine zilizopo zimeshachoka na ni za muda mrefu.

3. Wakala wa Majengo pia ina uchache wa wafanyakazi hususan katika kada ya masaramala na wataalamu wenye fani maalum za majengo katika ofisi zake kwa Unguja na Pemba. Wataalamu hao kama vile ‘Civil Engineers’, ‘Architects’, ‘Quantity Surveyors’, ‘Electrical Engineer’ pamoja na ‘Mechanical Engineer’.

4. Maslahi madogo kwa wataalam, hii husababisha hata vijana wanaomaliza masomo yao kuogopa kuajiriwa na Wakala wa Majengo kwani wanapokua

kwenye mazoezi ya vitendo (Field) hulipwa maslahi makubwa kutoka kwenye taasisi walizofanyia mazoezi ukilinganisha na maslahi wanayoyapata wenzao walioajiriwa Serikali.

### 2.6.2.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kushirikiana na Wizara husika kuharakisha upatikanaji wa maeneo ya kujenga ofisi za kudumu ya Wakala wa Majengo kwa upande wa Unguja na Pemba.

2. Kamati inaitaka Wizara pamoja na Wakala wa Majengo kuandaa mpango maalum wa kutoa elimu kwa wananchi, wawekezaji pamoja na makampuni juu ya umuhimu wa usajili kabla ya kuanza kutekeleza kwa miradi inayokusudiwa kutekelezwa ndani ya nchi yetu.

3. Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara wakati wa utekelezaji wa miradi mikubwa kutoa kipaumbele kwa kampuni za ujenzi za ndani ambazo ni za wawekezaji wetu wazalendo.

4. Kamati inaishauri Wakala wa Majengo kupitia Bodi inazozisimamia, kuandaa Muundo wa Utumishi kwa Ofisi na kupeleka Tume ya Utumishi Serikali ili kupata idhini ya kufanya uajiri wa wafanyakazi wa kudumu ili kuondokana na tatizo la wafanyakazi wa muda.

5. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi yake ya ZSSF kufanya malipo ya fidia kwa Wakala wa Majengo kwa eneo la Michenzani. Eneo ambalo hapo awali lilikuwa idara ya Ujenzi.

6. Kamati yangu inaitaka Wakala wa Majengo kuendelea kubaki katika jengo hilo na wasihame hadi ZSSF watakapowalipa fidia kutokana na kubomolewa na kuhamishwa kwenye jengo lao hapo Michenzani ili fidia hiyo iwawezeshe kujenga jengo lao wenyewe, au hadi hapo watakapota jengo jingine lenye hadhi yao.

7. Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka kiwango maalum cha chini ambapo iwe ni lazima kwa kazi za hizo za ndani kupewe Makampuni ya ndani ili kuwalinda wasije kupotea kutokana na kazi nyingi za Serikali hivi karibuni kupewa Makampuni ya Nje wakati kampuni za Wazalendo wanaziweza kazi hizo.

### 2.6.2.7 BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO NA BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI ZANZIBAR

Bodi hizi zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria na zinafanya kazi chini ya Wakala wa Majengo Zanzibar. Lengo kuu la kuanzishwa kwake ni kuhahakisha wakandarasi wote wanaofanya kazi nchini wanasajiliwa, kuhakikisha mkandarasi anafanya kazi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Bodi na katika daraja alilosajiliwa, kusajili miradi yote ya wakandarasi, kuhakikisha ujenzi wowote unaofanyika nchini kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wakandarasi unafuata viwango vya ujenzi, usajili wa wataalamu pamoja na kufanya ukaguzi wa majengo.

### 2.6.2.8 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BODI YA USAJILI WASANIFU WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO NA BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI ZANZIBAR

1. Kukosekana kwa wafanyakazi wa kudumu kunapelekea Bodi kufanyakazi zake bila ya ufanisi.

2. Bodi hazina ofisi za kudumu kwani hadi sasa wanakaa katika jengo la kuazima.

3. Bodi hazipati ruzuku yoyote kutoka Serikalini jambo ambalo linapelekea kutoweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

4. Kutokuwepo kwa Sera ya Ujenzi hali inayoisababishia utekelezaji mdogo kwa Bodi hizi.

5. Bodi zinapata usumbufu katika kusajili wataalamu wanaokuja kufanya kazi kwa miradi ya ujenzi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na hatimae kupelekea miradi kutojulikana ubora na usalama wake na Sheria za Bodi kukiukwa.

6. Ukosefu wa Jumuiya ya fani ya ujenzi ambayo ingesaidia kuwakusanya na kutatua changamoto za wanataaluma wa fani ya ujenzi.

7. Wataalamu waliosajiliwa kuchelewa kulipa ada ya mwaka.

8. Mapungufu ya Sheria tulionayo kutokana na Sheria hiyo haikutaja ushirikishwaji wa Wahandisi katika fani ya barabara na nyenginezo.

9. Kutojisajili kwa wataalamu wa kigeni katika bodi husika hali inayopelekea kukosekana kwa mapato Seriakali.

### 2.6.2.9 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo kwa kuweza kufanikisha kuwasilisha ndani ya mwezi wa Oktoba - Disemba kiasi cha mapato yapatayo Tshs. Milioni 21,227,120 kwa Serikali.

2. Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara husika kuwapatia eneo kwa ajili ya kujenga jengo la ofisi zao za kudumu za Bodi hizo pamoja na kuwapatia fursa za kuajiri wafanyakazi wa kudumu.

3. Kamati inaitaka Idara ya Mipango kuharakisha upatikanaji wa Sera ya Ujenzi itakayoweka miongozo wa uwepo wa jumuia ya wataalamu wenye fani ya Ujenzi ambayo itasaidia kuwatambua lakini pia kuongeza mapato kwa Bodi.

4. Kamati yangu inaitaka Serikali kuwalazimisha wakandarasi wa kigeni kabla ya kuanza kazi zao hapa Zanzibar kuhakikisha wanasajiliwa katika Bodi ili kuweza kupimwa uwezo wao pamoja na kuhakikisha kuwa ujenzi unaofanywa ndani ya Zanzibar unakuwa na viwango bora.

### 2.6.3 **SEKTA YA NCHI KAVU**

Katika ripoti hii, Kamati inazijumuisha Idara ya Utunzaji na Uendelezaji wa Barabara (UUB) pamoja na Idara ya Usafiri na Leseni ni miongoni mwa usafiri wa nchi kavu.

#### 2.6.3.1 **IDARA YA UTUNZAJI NA UENDELEAJI BARABARA (UUB)**

Idara ya Utunzaji na Uendelezaji Barabara ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ambayo inafanya kazi za kujenga na kuzitunza barabara za visiwa vya Unguja na Pemba. Hali ambayo inapelekea kupatikana kwa mafanikio mbalimbali ikiwemo miundombinu bora ya barabara inayopitika muda wote wa misimu ya mwaka pamoja na kupungua kwa gharama za usafirishaji mizigo na abiria.

Aidha, Idara hii pia kwa sasa inasimamia mradi wa kukuza sekta ya usafiri nchini (TSSP) ambao unajumuisha barabara zifuatazo:

(a) Barabara ya Bububu, Mahonda kupitia Kinyasini hadi Mkokotoni.
(b) Barabara ya matemwe – Muyuni.
(c) Barabara ya Pale (Donge) hadi Kiongele (Mkwajuni.
(d) Barbara ya Fuoni hadi Kombeni.

#### 2.6.3.2 **CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI IDARA YA UENDELEZAJI NA UTUNZAJI BARABARA (UUB)**

1. Uchakavu wa Mitambo na zana za kufanyia kazi inayorudisha nyuma maendeleo ya ujenzi barabara nchini.

2. Ugatuzi wa Madaraka unapelekea upotevu wa fedha nyingi za Serikali pamoja na kusababisha kasi ya utendajikazi kupungua.

3. Ukosefu wa posho nyeti kwa wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

4. Ucheleweshaji wa uingizwaji wa fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwenda Idara ya Utunzaji na Uendelezaji wa Barabara.

5. Uhaba wa fedha za matengenezo ya barabara kwa upande wa Unguja na Pemba.

6. Ukosefu wa utaalamu kwa wakandarasi wazalendo wanaoshirikishwa katika kazi za matengenezo ya barabara.

7. Ucheleweshaji wa ulipaji fidia kwa wananchi walioathirika katika ujenzi wa barabara zikiwemo nyumba na vipando jambo ambalo linapelekea kushindwa kutekelezwa kwa baadhi ya miradi.

8. Matumizi yasiyotarajiwa hasa zinaponyesha mvua na ziara za viongozi Wakuu wa Nchi husababisha matumizi nje ya Bajeti iliyopangwa na kusababisha kazi nyingine zilizopangwa kuchelewa.

### 2.6.3.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kushirikiana na Wizara kuweza kuharakisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Barabara “ZANROAD”.

2. Kamati inashauri Wizara kupitia Idara ya Utunzaji na Uendelezaji wa Barabara (UUB) kuendelea na Utoaji wa Elimu kwa wananchi juu ya hifadhi ya maeneno ya Barabara.

3. Kamati pia inaipongeza Wizara kupitia Idara ya Utunzaji na Uendelezaji wa Barabara kwa kuanzisha Bima ya Afya kwa

wafanyakazi wake na kujitolea kwa kuchangia kwa kila mfanyakazi asilimia 6 ya mshahara wake.

4. Kamati inaiomba Serikali kupitia Idara ya Mipango kuharakisha ununuzi wa mitambo ya kisasa iliyobora ili Idara iweze kukamilisha miradi waliyoianza na mingine inayoendelea.

5. Kamati inaitaka Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kuwapatia posho wafanyakazi wanaofanyakazi katika mazingira magumu ili kuwapa moyo na kuongeza morali ya kufanya kazi.

6. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuitia nguvu Idara (UUB) kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

7. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mfuko wa Barabara kuacha urasimu wa kutoa fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Barabara kwani fedha wanazokusanya madhumuni yake ndio hayo na sio kitu kingine isipokuwa kuzienzi na kuzihami barabara zetu.

8. Kamati inaiomba tena Serikali kusomesha wataalamu wetu wa ndani ili waendane na mifumo mipya ya Sayansi na teknolojia hususan katika matumizi ya mitambo na vifaa vya kisasa.

### 2.6.4 **SEKTA YA USAFIRI WA MAJINI**

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano inairipoti Sekta hii kuwa inajumuisha Shirika la Bandari, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA) na Shirika la Meli na Uwakala.

#### 2.6.4.1 **SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR**

Kamati inatambua kwamba Shirika la Bandari linajukumu la kuziendesha, kuzisimamia na kuziendeleza Bandari tano za Zanzibar ambazo ni Bandari ya Malindi, Mkokotoni, Wesha, Mkoani na Wete.

Sambamba na hilo, Kamati katika kufanya kazi zake walizopangiwa, imebaini kwamba licha ya mfanikio mengi yaliopatikana kupitia Shirika hili bado kuna maeneo kumi na tatu (13) ambayo yapo katika umiliki wa Bandari hayana hatimiliki kutoka Serikalini. Miongoni mwa maeneo hayo kwa upande wa Unguja na Pemba ni kama yafuatayo:

(a) Bandari ya Malindi.
(b) Bandari ya Mkoani.
(c) Bandari ya Wesha.
(d) Bandari ya Wete.
(e) Bomani Guest House.
(f) Eneo la Mnara wa Matumbilini.
(g) Eneo la Mnara wa Chumbe.
(h) Eneo la Mnara wa Mbao (kilimani).
(i) Eneo la Mnara wa Nungwi.
(j) Eneo la Mnara wa Pungume.
(k) Eneo la Mnara wa Mangapwani.
(l) Eneo la Mnara wa Makunduchi.
(m) Nyumba ya Bopwe Pemba.

### 2.6.4.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR

1. Kukosekana kwa hatimiliki katika Bandari zote za Serikali kwa upande wa Unguja na Pemba hali inayopelekea wananchi kuvamia pamoja na kujimilikisha maeneno hayo kinyume na taratibu.

2. Uvamizi pamoja na ujenzi holela katika maeneo ya minara ya kuongozea meli. Mfano, mnara wa Nungwi.

3. Kutokuwepo kwa eneo maalum la kuwekea na kuhifadhia makontena ambayo yanasubiria kupakiwa melini.

4. Madeni makubwa wanayodai kutoka Tanzania Port Authority yanayotokana na huduma za utumiaji wa minara na maboya kwa meli zinazokwenda Tanzania Bara.

5. Kuchelewa kwa malipo ya huduma zinazotolewa kwa baadhi ya Makampuni na Mashirika yakiwemo ‘Azam Marine’ na Shirika la Meli la Zanzibar. Hivyo, kupelekea kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu kwa Shirika.

**TAWI LA PEMBA**

Tawi la Shirika Pemba ni moja kati ya Idara sita katika muundo wa Shirika la Bandari Zanzibar, likiwa na majukumu ya kusimamia shughuli zote za kiutawala na uendeshaji wa kazi kwa upande wa Pemba kupitia Bandari tatu (3) ambazo ni Bandari ya Mkoani, Wete na Wesha.

Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Septemba, Tawi hili lilikusanya mapato yenye jumla ya Tshs. 237,028,687.95 sawa na asilimia 36.23 ya ongezeko la Tshs. 63,037,902.49.

### 2.6.4.3 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA BANDARI TAWI LA PEMBA

1. Kutokuja kwa meli za kigeni za mizigo kutoka nje ya Nchi ikiwemo makontena na mizigo mengineyo mchanganyiko licha ya juhudi na jitihada za uwekezaji zinazoendelea kufanyika katika Bandari ya Mkoani. Hali hiyo inapelekea kutofikiwa kwa malengo ya Tawi.

2. Uvamizi wa maeneo ya Bandari unaoendelea kufanywa na wananchi kwa kujenga majengo ya makaazi pamoja na biashara.

3. Ukosefu wa hati miliki ya maeneo mengi ya Bandari za Pemba.

4. Kuchelewa kwa malipo ya huduma zinazotolewa kwa baadhi ya Makampuni na Mashirika yakiwemo ‘Azam Marine’ na Shirika la Meli la Zanzibar. Hivyo, kupelekea kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu.

5. Mazingira ya Bandari ya Pemba yanasumbua katika udhibiti kutokana na matumizi ya Bandari hizo kwa wakaazi wa Visiwa pamoja na hali ya watu kuweza kuingia wakati maji yanapotoka.

6. Upungufu wa wafanyakazi katika kada mbali mbali kutokana na baadhi ya wafanyakazi kustaafu kwa kufikia umri wa lazima.

### 2.6.4.4 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kukamilisha zoezi zima la upatikanaji wa hatimiliki kwa maeneo yote ya Bandari na Minara kwa Unguja na Pemba. Ili kuweza kuyahami maeneo hayo na uvamizi unaoendelea kushamiri unaofanywa na wananchi kwa kujenga makaazi pamoja na kufanya sughuli zao za kibiashara katika maeneo hayo.

2. Kamati pia inaiomba tena Serikali kuweza kuwapatia Shirika la Bandari eneo la kudumu la Maruhubi ili kuweza kuweka makontena na hivyo kuondokana na changamoto ya msongamano wa makontena katika eneo la bandari pamoja na Bwawani.

3. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Bandari kuanza ujenzi wa kuweka ukuta katika maeneo yote ya Bandari kwa Unguja na Pemba ili kuzihami na matokeo ya uvamizi unaokiuka taratibu za kisheria.

4. Kamati inalitaka Shirika la Bandari kufanyakazi kwa pamoja na ZMA ili kuweza kutoa takwimu zilizo sahihi na bila ya utofauti wowote za uingiaji wa meli na majahazi ili kunusuru upotevu wa mapato kwa Serikali pamoja na usafirishaji wa mizigo.

5. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Bandari pamoja ZURA kuweka ‘Floor Metre’ katika Bandari ya Wesha wakati wa meli za mafuta zinapokuwa zinashusha.

6. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Ofisi za Halmashauri, Wilaya na Masheha kuyalinda maeneo ya Bandari kwa upande wa Unguja na Pemba na kutotoa vibali vya ujenzi katika maeneo hayo bila ya idhini ya Waziri anayehusika na masuala hayo.

7. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Shirika husika kuandaa mpango maalum wa kuwapatia elimu vikundi vyote vya ushirika vinavyofanya kazi katika Shirika la Bandari kupitia Jumuiya zao.

8. Vilevile, Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa ndani wa Wizara kupitia Taasisi husika pale inapotokezea kutekelezwa kwa mradi unaohusu Wizara au Taasisi husika ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa mradi huo.

### 2.6.4.5 **MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA)**

Mamlaka ya Usafiri Baharini imeanzishwa chini ya Sheria namb.3 ya mwaka 2009. (Zanzibar Maritime Authority Act No. 3 of 2009). Aidha, Mamlaka inafanya kazi zake za kila siku chini ya Sheria ya Usafiri Baharini (Maritime Transport Act No. 5 of 2006).

Majukumu makuu ya Mamlaka hii ni kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini, kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya manahodha, kusimamia shughuli za upakiaji wa abiria katika bandari za Zanzibar kwa mashirikiano na Taasisi nyengine husika, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya baharini na utekelezaji wa kanuni ya kimataifa ya ulinzi wa meli na bandari.

Sambamba na hilo, Mamlaka pia ina jukumu la kusimamia safari za baharini, uchunguzi wa ajali baharini, uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa maeneo ya Zanzibar, usimamizi wa maslahi ya mabaharia pamoja na kusajili na kutoa vibali na leseni kwa taasisi zinazotoa huduma za meli na bandari.

### 2.6.4.6 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YAUSAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA)

1. Kuzorota kuridhiwa kwa mikataba ya kimataifa ya usimamizi wa usafiri baharini. Jambo hili linapelekea bendera yetu kuonekana haiko makini katika kusimamia usajili wa meli.

2. Kukabiliwa na ukaguzi wa IMO. Pamoja na kuwa Tanzania kuna taasisi mbili zinazosimamia usafiri baharini, hivyo kwa kiasi kikubwa ukaguzi huo unalenga kuikagua ZMA kwani ndiyo inayosajili meli za nje.

3. Kusitishwa kwa zoezi la usajili wa meli za nje kufuatia meli zilizokamatwa ambazo zilisajiliwa Zanzibar na kupokea Agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo kupelekea kusimama kwa ufanyajikazi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) katika suala zima la usajili wa meli za nje jambo linalosababisha kupunguza vianzio vya makusanyo ya Serikali.

4. Kutokuwepo kwa mkataba wa uwakala kati ya ZMA na Kampuni ya ZIMS. Hii inapelekea ZIMS kuendesha shughuli za usajili wa meli kinyume na taratibu za UAE. Hii inatokana na ukweli kwamba, kwa mujibu wa kanuni za UAE, kampuni binafsi iliyosajiliwa nchini humo haiwezi kuendesha

shughuli za nchi nyengine bila ya kuwa na mkataba na uwakala kutoka taasisi ya nchi husika.

5. Kutokuwepo matayarisho ya usajili wa “VAT” ambapo kuanzia mwezi Januari, 2018, Serikali ya UAE imeanza kutoza kodi kwa biashara mbalimbali zinazoendeshwa nchini humo. Aidha, ZIMS hadi kufikia sasa haijafanya usajili wa kodi ya “VAT” kwa sababu inasubiri mkataba wa uwakala baina ya ZMA na ZIMS ambao upo katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali unafanyiwa kazi tangu tarehe 22 Novemba, 2017 na kuchelewa kumalizika kwa suala hilo, kutapelekea ZIMS kutozwa faini au kufungiwa.

6. Kukosekana kwa vyombo vya kudumu vya uokozi baharini hali inayoweza kupelekea kushindwa kudhibiti janga lolote linaloweza kutokea katika nchi.

**TAWI LA PEMBA**

Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) Tawi la Pemba pia ina majukumu ya kusimamia usalama wa vyombo vya abiria vya baharini na kusimamia idadi ya abiria wanaosafiri kwa kutumia vyombo hivyo pamoja na mizigo yao kwa mujibu wa Sheria. Ofisi ndogo ya Pemba pia ina jukumu la kufanya ukaguzi wa vyombo vidogo vidogo ili kuhakikisha vinasajiliwa na vinafuata taratibu zilizowekwa na Sheria.

### 2.6.4.7 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA) TAWI LA PEMBA

1. Ukosefu wa mafunzo ya vitendo ya muda mfupi na mrefu kwa watendaji wa Mamlaka kwa upande wa Pemba.

2. Kutokua na kituo cha Ofisi cha ZMA katika bandari ya Wesha na Wete hali ambayo inapelekea wafanyakazi wa Mamlaka hii kulazimika kujibanza katika taasisi nyengine wakati wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

3. Uhaba wa watendaji katika vituo vya ukaguzi ambapo katika Bandari ya Wete kuna mfanyakazi mmoja na katika Bandari ya Wesha kuna mfanyakazi mmoja hali ambayo inapelekea ukosefu wa huduma pamoja na kuikosesha mapato Serikali.

4. Ukosefu wa vyombo maalum vya ufuatiliaji wa vyombo vidogo vidogo vikiwa baharini hususan wakati wa usafirishaji vitu kinyume na taratibu za Sheria.

5. Uhaba wa bajeti kwa Ofisi ya Kituo cha ZMA (Pemba).

6. Ukosefu wa mtu wa hesabu katika Ofisi ya Kituo cha ZMA (Pemba).

7. Ukosefu wa Jengo la Ofisi Kuu ya ZMA (Pemba).

8. Ukosefu wa muundo wa kiofisi na kiitumishi.

### 2.6.4.8 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kuiagiza Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuharakisha upatikaji wa mkataba wa uwakala baina ya ZMA na ZIMS ili kulinusuru Tawi la Dubai kuja kutozwa faini na kufungiwa kwa kufanya kazi kinyume na taratibu za nchi.

2. Kamati inaishauri Wizara pamoja na Mamlaka husika kutafuta eneo la kujenga jengo la ofisi za ZMA za kisasa zinoendana na hadhi ya jana lao. Kwani hapo walipo ni eneo dogo na halikidhi haja.

3. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikana na Mamlaka ya Usafiri Baharini kutafuta mbinu mbadala zitakazoweza kuwaongezea ujuzi watendaji waliopo katika Ofisi za ZMA Pemba.

4. Kamati pia inaitaka Mamlaka ya Usafiri Baharini kusimamia majukumu yao ipasavyo ili kuepusha upotevu wa pato la Serikali kupitia vyombo vya usafiri baharini pamoja na kudhibiti usafirishaji wa bidhaa kimagendo.

5. Kamati inaishauri Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini kuweza kuhakikisha kuwa vyombo vyote vinasajiliwa ili kulinda usalama wa nchi yetu na Taifa kwa ujumla.

6. Kamati inaitaka Wizara kukaa pamoja na Mamlaka ya Usafiri Baharini kutoa elimu kwa jamii husika kabla ya kuletwa kwa boti zitakazotumika kwa usafiri wa ndani katika Visiwa vya Fundo na Gando (Pemba).

7. Kutokana na Changamoto mpya zilizoanza kujitokeza kwenye usajili wa Meli za Nje hasa kukiuka Sheria za Kimataifa ikiwemo kupakia magendo ya silaha pamoja na madawa ya kulevya, ni vyema kwa ZMA kuzungumza na Makampuni ya Meli tuliyofunga nayo mikataba kuheshimu makubaliano hayo lakini pia kuweka masharti magumu kwa Meli mpya ambazo tunazisajili kwa kipindi hiki.

### 2.6.4.9 **SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR**

Shirika la Meli Zanzibar limepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia bandari za Zanzibar. Aidha, Shirika linatoa huduma bora za usafirishaji wa abiria na mizigo baina ya Visiwa vya Zanzibar na kwengineko na kusimamia biashara ya meli kama mmiliki, dalali, wakala wa Kampuni za meli za kigeni zinazofanya biashara hapa Zanzibar.

Shirika kupitia programu ndogo ya huduma za usafirishaji limetoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni 113 zinazoingia nchini. Kupitia meli yake ya MV Mapinduzi II, limefanya safari 24 kwa kipindi cha miezi mitatu na kuhudumia

jumla abiria 49,734 pamoja na kuhudumia tani 4,974 za mizigo ikiwemo magari na mizigo mengineyo.

### 2.6.4.10 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA BANDARI

1. Kwa upande wa meli ya MV Mapinduzi II, changamoto kubwa inayojitokeza ni usimamiaji na uendeshaji wa meli hiyo unaotokana na uharibikaji wa mara kwa mara unaopelekea kushindwa kufanya kazi zake kikawaida.

2. Kukosa wataalamu wazalendo wa kudumu wa kushughulikia meli hiyo mara tu tatizo linapojitokeza.

3. Ufatiliaji wa vipuri vinavyopatikana nje ya nchi jambo linalopelekea kuchelewa kurudi meli hiyo katika hali ya kawaida wakati inapoharibika.

4. Kukosekana kwa ushirikishwaji wa watendaji katika hatua za mchakato mzima wa manunuzi ya Meli mpya zinazokubaliana na hali ya hewa Zanzibar.

### 2.6.4.11 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI.

1. Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara husika kupitia Shirika la Meli Zanzibar kutafuta meli nyengine mbadala itakayoendana na mazingira ya visiwa vyetu na kuondosha usumbufu pindipo meli ya MV Mapinduzi II itapokumbwa na tatizo.

2. Kamati inaipongeza Wizara kupitia Shirika la Meli kwa uuzaji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki jambo linalopelekea kuepusha wasafiri hewa.

3. Pia Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Shirika kusomesha wataalamu ili waweze kuendana na Technologia mpya ya Meli zinazokuja

ili kuweza kuzielewa na kuzikabili changamoto za kiuendeshaji na kiufundi zinapotokea.

4. Kwa kuwa tunazo taarifa za mipango ya Serikali kununua Meli nyingine mpya ya abiria, Kamati inaiomba Serikali pamoja na Wizara husika kuanza kusikiliza maoni ya wataalamu wa Shirika juu ya aina ya Meli tunayoihitaji na ambayo itaendana na maazingira ya bandari zetu na pia wasafiri wetu.

### 2.6.5 SEKTA YA ANGA

#### 2.6.5.1 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria namba 9 ya mwaka 2011, ambayo awali ilikuwa ikijulikana kama Idara ya Anga. Aidha, Mamlaka inaendesha, inasimamia usalama kwa safari za abiria na mizigo na kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Serikali kikiwemo Kiwanja cha Kimataifa cha Amani Abeid Karume cha Unguja na Kiwanja cha Ndege cha Pemba.

Mamlaka katika kuimarisha huduma za usafiri wa anga Zanzibar, inaendelea na utaratibu wa kujenga viwanja vya helkopta katika eneo la Domokuchu, Paje na Kigomasha, pamoja na kujenga njia ya kurukia na kutulia ndege ndogo (Airsrip) Kigundu, Nungwi kwa Unguja na kwa Pemba njia hiyo inajengwa huko Mkoani.

#### 2.6.5.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE

1. Kuzidiwa na jengo la abiria linalotumika hivi sasa, hali ambayo inapelekea mrundikano wa abiria pamoja na kuwepo joto kali katika sehemu za kuwasili na kuondokea abiria.

2. Kutokuwepo kwa mashine za kukagua mizigo mikubwa katika Kiwanja cha ndege cha AAKIA pamoja na upungufu wa mashine za kukagulia abiria na mizigo midogo midogo, hali inayopelekea baadhi

ya mashirika ya ndege kukataa kabisa kubeba mizigo kutoka Zanzibar.

3. Udhaifu katika Huduma za kiwanja, hii inatokana na kukosekana kwa mikanda ya mizigo (Conveyer belt), pamoja na kutokuwepo kwa idadi na taarifa kamilifu za abiria pale zinapohitajika.

4. Gharama kubwa kwa mafunzo ya sekta ya usafiri wa anga yanapelekea mamlaka kutumia sehemu kubwa ya mapato yake kwa ajili ya kuwasomesha wafanyakazi wake, hasa ukizingatia mafunzo mengi yanayotekelezwa na Mamlaka yanalazimika kisheria ikiwemo kuwapeleka wafanyakazi kupatiwa leseni.

5. Gharama kubwa za umeme ambapo kwa mwezi Mamlaka inalazimika kulipa umeme wa wastani Tshs. 80 Milioni, ambapo 55 Milioni bili la mwezi na 25 Milioni malipo ya deni la nyuma, hali ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa cha mapato yanayopatikana.

6. Uchache wa wafanyakazi wa Usalama. Hii inatokana na Mamlaka kufanya kazi kwa masaa 24, utanuzi wa maeneo, kuongezeka abiria, ndege na mizigo hivyo kupelekea kuhitajika kwa wafanyakazi zaidi ili kukidhi utendaji kwa mujibu wa utaratibu wa utumishi na sheria za kiusalama katika safari za ndege.

### 2.6.5.3 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuimarisha maeneo ya kupitishia mizigo (Conveyer belt) ili kuondosha usumbufu kwa abiria hususan wakati wa kushuka.

2. Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Mamlaka kuliangalia kwa makini suala la “scanner” ambalo hutumiwa na wafanyakazi kupitisha mizigo tofauti.

3. Kamati inaishauri Wizara kutafuta mbinu mbadala za kutafuta umeme wa solar ili kupunguza gharama za umeme zisizo za lazima katika Viwanja vya ndege kwa Unguja na Pemba.

4. Kamati inaiomba Wizara kufanya jitihada za kumaliza jengo la Uwanja wa Ndege la ‘Terminal II’ kwa muda wa miezi 18 ili kutimiza ahadi za Mheshimiwa Rais kabla ya kumaliza muda wake wa kuwatumikia wananchi wa Taifa hili.

5. Kamati inaishauri Wizara kutowazuia wafanyakazi ambao wanamalengo ya kuendelea kusoma zaidi hasa katika ngazi za utaalamu.

6. Kamati inaishauri Wizara kuwashirikisha kikamilifu watendaji wetu wa ndani wa Mamlaka ya Viwanja wa Ndege katika Ujenzi wa Mradi wa Terminal II kwa wao ndio wahusika wakuu katika utumiaji wa jengo hilo baada ya kukamilika kwa ujenzi huo.

7. Kamati yangu inaishauri Serikali Kuangalia uwezekano wa kuwahamisha wananchi waliojenga pembezoni mwa Uwanja wa Ndege ‘Terminal II’ ili ipatikane “Bufferzon” angalau mita 60 kwa usalama wa Ndege zitakazokuja kuegesha katika kiwanja hicho.

8. Kamati vile vile inaishauri Serikali kuwa jengo la ‘Terminal II’ litumike kwa ajili ya abiria wa “International Flights” tu na wale wa local waendelee kutumia Uwanja huu wa sasa ili kukidhi nafasi kwenye jengo hilo.

## 2.6.6 **SEKTA YA MAWASILIANO**

### 6.6.6.1 **IDARA YA MAWASILIANO**

Idara ya Mawasiliano Zanzibar ina jukumu kuu la kusimamia na kutoa miongozo katika mambo yote yanayohusiana na Tehama, Zanzibar ambapo, kuanzia mwaka 2013 kupitia Sera ya Tehama, Zanzibar idara hii imefanikiwa kujenga vituo vya Tehama Jamii katika Wilaya kumi (10) zilizopo Unguja na Pemba. Navyo ni:

(a) Wilaya ya Mjini Magharibi B - Kiembe Samaki.
(b) Wilaya ya Mjini Magharibi A - Mwera Wilayani.
(c) Wilaya ya Kusini - Kitogani karibu na holi la CCM.
(d) Wilaya ya Kati - Tunguu.
(e) Wilaya ya Kaskazini A - Mkabala na Kituo cha Polisi cha Mkokotoni.
(f) Wilaya ya Kaskazini B - Mahonda.
(g) Wilaya ya Wete - Jadida Chekechea.
(h) Wilaya ya Mkoani - Mtambile.
(i) Wilaya ya ChakeChake - Machomane.
(j) Wilaya ya Micheweni - Nyuma ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

### 2.6.6.1 **CHANGAMOTO ZINAZOVIKABILI VITUO VYA TEHAMA JAMII**

1. Ukosefu wa vyoo katika majengo yote ya Vituo vya Tehama Jamii kwa upande wa Pemba.

2. Ukosefu wa viyoyozi katika vituo vyote vya Pemba.

3. Ukosefu wa Hatimiliki ya maeneno yote ya Vituo.

### 2.6.6.2 **MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano, Zanzibar kuharakisha zoezi la upatikanaji wa hatimiliki katika maeneo hayo ya vituo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika.

2. Kamati inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Idara husika kuviwekea bajeti maalum ya kuviendeleza vituo hivyo.

3. Kamati inaiomba Wizara pamoja na Idara husika kuzienzi na kuzitunza mali za Serikali kwa manufaa ya jamii kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

4. Kamati pia inaishauri Idara kuhakikisha madhumuni ya kujengwa kwa vituo hivyo yanafikiwa kwa walengwa husika bila ya ubaguzi wowote na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuanzishwa kwake.

5. Kamati pia inaiomba idara kukaa pamoja na Shirika la Umeme (ZECO) kuweza kuona kwa namna gani wanaweza kuwasogezea huduma za uuzaji umeme katika maeneo yote ya Vituo hususan kwa upande wa Pemba na Unguja.

# SEHEMU YA TATU

## 3. HITIMISHO

Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi inawashukuru sana Watendaji wote wa Wizara pamoja na Taasisi zote za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa kuweza kutoa mashirikiano makubwa ya kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa mwaka huu 2017/2018. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata cha Kamati.

Hata hivyo, kasoro kubwa iliyogunduliwa na Kamati ni **Upatikanaji mdogo wa fedha za OC kwa wakati kutoka serikalini** ambao umekwamisha kwa kiasi kikubwa malengo na shabaha za Wizara zote mbili zinazosimamiwa na Kamati hii hasa katika miradi ya Maendeleo na kazi za kawaida.

Vilevile, upatikanaji wa fedha za OC, vitendea kazi pamoja na usafiri navyo ni miongoni mwa mambo yaliyopelekea kukwamisha na kurudisha nyuma mwamko na ufanisi wa kazi za watendaji wetu.

## 3.1 MAPENDENDEKEZO NA MAAGIZO YA KAMATI KWA SERIKALI

Kamati inaiagiza Serikali kuzipatia Wizara hizi fedha za Bajeti pamoja na fedha za OC kwa wakati ili kurahisisha utekelezaji wa malengo yaliopangwa wa wakati.

Mwisho kabisa na kwa umuhimu mkubwa, Kamati inapenda kutoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Raya Issa Msellem pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na umahiri mkubwa.